OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI TARIME

SHULE YA SEKONDARI BOMANI,
S.L.P 363,
TARIME.
Mob +255 755569245
bomanisecondary20@gmail.com

10/12/2021

KUMB.NA. TRM/BM/S.S/J.I/VOL 1/11

JINA LA MWANAFUNZI

_____

S.L.P_____

_____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BOMANI HALMASHAURI YA MJI TARIME MKOA WA MARA MWAKA 2022

UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, katika shule hii mwaka 2022. **Hongera sana**

Shule ya sekondari Bomani ipo umbali wa km 2½ toka Tarime Mjini mtaa wa Buhemba, kata ya Bomani. Shule hii ni ya kutwa ya mchanganyiko wa wasichana na wavulana. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **17/01/2022** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **17/01/2022** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **17/02/2022**. Kila mwanafunzi aje na mzazi/mlezi wake saa 2:00 asubuhi kwa **USAJILI.** Mahitaji na vifaa vyote vya shule vitakaguliwa siku ya kuripoti

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

A: SARE YA SHULE

i. **Wavulana.**
   - Suruali mbili zenye mifuko mitatu zisizo na madoido yoyote (moja nyeusi naya pili damu ya mzee). Upana chini **usipungue sentimeta 18** na iwe na pindo (turn up) kitambaa ni **ISTIM namba moja**.
   - Shati nyeupe mbili mikono mifupi (Tetron) zisiwe zinazobana mwili.
   - Sweta la blue lenye "V" shingoni.
   - Viatu vyeusi vya kamba visivyo na madoido yoyote.
   - Soksi nyeupe jozi mbili.
   - T-shirt ya shule

ii. **Wasichana.**
   - Sketi mbili zenye; zenye marinda na urefu wa kufunika magoti (***inchi 12 kutoka kwenye magoti kwenda chini***) upana wa pindo la tumboni uwe inchi mbili: moja **nyeusi** yenye michirizi wa kijani na ya pili **damu ya mzee** yenye michirizi myeupe. "SKETI ZOTE ZIWE ZA KITAMBAA KIZITO" (TUNASISITIZA ZISIWE FUPI) Kitambaa ni **ISTIM namba moja**
   - Shati nyeupe mbili mikono mifupi (Tetron) zisiwe za kubana
   - Sweta la blue lenye "V" shingoni.

- Viatu vyeusi vya kamba visivyo na madoido yoyote.
- Soksi nyeupe jozi mbili ndefu zinazofika magoti (stocking)
- T-shirt ya shule

N.B: Wanafunzi wasichana wa KIISLAMU watavaa sketi ya marinda, ndefu inayofunika miguu na blauzi nyeupe mikono mirefu (half kanzu) na kitambaa cha kichwani (Hijabu rangi nyeupe) isiyo na urembo wowote.

Sare ya michezo kwa shule hii ni **tracksuit ya rangi ya bluu bahari (Light blue)** kwa wavulana na wasichana isiwe inayobana mwili. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na viatu (raba) vya michezo

B. MAHITAJI BINAFSI YA DARASANI.

I. Mathematical set (mkebe wa hesabu) wa mwanafunzi wa sekondari
II. Madaftari makubwa **Quire 2 au Quire 3** yawe tisa
III. Begi la kubebea madaftari
IV. Kalamu ya wino blue au nyeusi tano
V. Penseli
VI. Rula moja
VII. File moja yenye spring tags kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi
VIII. Picha nne (04) za rangi passport size
IX. Njoo na nakala moja ya cheti cha kuzaliwa.

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi,yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais-**TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi katika kiambatanisho 'A', 'B' na 'C'

KIAMBATANISHO 'A'

Unatakiwa kusoma mambo haya ya msingi, kisha utaweka saini yako pamoja na mzazi/mlezi wako kuonyesha kuwa umeelewa na kukubaliana nayo. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni ikiwa imesainiwa na mwanafunzi pamoja na mzazi/mlezi wake.

KIAMBATANISHO 'B'

Hii ni fomu ya maelekezo ya uchunguzi wa Daktari kuhusu hali ya afya ya mwanafunzi. Fomu hii ijazwe na Daktari/Mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

KIAMBATANISHO 'C'

Fomu ya URAIA - Leta photocopy ya cheti cha kuzaliwa au jaza AFFIDAVIT FORM toka ofisi ya Mkuu wa Wilaya

KARIBU SANA BOMANI SEKONDARI

.....
MWL. BAKENGESA JAMES
MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI BOMANI

FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE

1. TAARIFA ZA MWANAFUNZI

a) Jina kamili la mwanafunzi ……
b) Tarehe ya kuzaliwa …….
c) Mahali anapoishi (Mtaa/kata) ……
d) Uraia; MTANZANIA/ SI MTANZANIA …….
e) Shule aliyotoka ……..

2. TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

a) Jina la mzazi/mlezi ……
b) Kazi ya mzazi/mlezi……
c) Anuani ya mzazi/mlezi ……...
d) Mahali anapoishi mzazi/mlezi ……...
e) Namba ya simu ……...
f) Ndugu/Jmaa wa karibu wa mwanafunzi. (Jaza jedwali lifuatalo)

Na	Jina la ndugu/Jamaa	Anapoishi	Uhusiano	Namba ya simu
i				
ii				
iii				

3. AHADI/KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi ……nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote ya kujiunga na shule ya sekondari BOMANI. Ninaahidi kufata maelekezo yote, sharia na taratibu zote za shule. Sitashiriki wala kujihusisha na migomo, fujo wala makossa ya jinai. Endapo nitakiuka kiapo hiki uongozi wa shule uchukue hatua za kinidhamu juu yangu.

Sahihi ……. Tarehe …….

4. AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi ……... mzazi/mlezi wa mwanafunzi ninakiri niko tayari kupokea uamuzi utakaotolewa na shule endapo mwanafunzi atavunja sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi ya mwanangu muda wote wa masomo yote ikiwa ni pamoja na kufatilia maendeleo yake kitaaluma. Nitampatia mahitaji yote mhimu kama uongozi wa shule utakavyokuwa ukielekeza.

Sahihi ya mzazi/ Mlezi …… Tarehe……

KIAMBATISHO "A"

I. <u>MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA.</u>

1. Kuvuta sigara/bangi
2. Kufuga kucha ndefu na nywele ndefu zisizotuzwa katika hali ya usafi
3. Kufuga ndevu
4. Kuvaa sare isiyo na heshima ya kubana na fupi
5. Kugombana
6. Kuiga mitindo ya kihuni kama kunyoa kipara,kupaka kucha rangi, kuvaa mavazi ya kubana mwili au mafupi n.k.
7. Kuchubua ngozi ya mwili kwa kutumia madawa
8. Wageni wa wanafunzi hawaruhusiwi kuwasiliana nao pasipo idhinii ya uongozi wa shule walimu/mwalimu wa zamu.
9. Kwenda nje ya shule bila ruhusa wakati wa masomo.
10. Kuvaa kofia,bangili na mapambo mengine yoyote.
11. Kutohudhuria shule (masomo) bila ya kuwa na ruhusa au taarifa shule.
12. Kuwa na nywele fupi zinazotunzwa vizuri. Aidha mwanafunzi haruhusiwi kusuka, kufuga ndevu na kunyoa kipara au kiduku.

II. <u>MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI:-</u>

1. Wizi.
2. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya/mihadharati.
3. Uasherati, ubakaji na ushoga.
4. Uvutaji bangi.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana na kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa.
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kutoroshwa au kutorosha
13. Kugoma au kuchochea na kuongoza fujo zenye kuvuruga amani na usalama wa watu na shule
14. Kukataa adhabu kwa makusudi.
15. Kupatikana na simu ya viganjani (mobile phone) shuleni.

III. <u>MAMBO AMBAYO KILA MWANAFUNZI ANAPASWA KUYAFANYA.</u>

1. Kufuata taratibu zote kama zitakavyoonyeshwa katika ratiba ya shule na kama zitakavyokuwa zinatolewa na viongozi.
2. Kuwa na utii na heshima kwa walimu,wafanyakazi wa shule viongozi na raia wote kwa ujumla.
3. Kuheshimu Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa na wa shule.
4. Kulinda maadili yaliyo katika kauli mbiu ya shule- "**Struggle for Success"**
5. Kutumia lugha ya kiingereza daima wakati wote wa saa za masomo na kuwasiliana ndani ya mazingira ya shule.
6. Kuzingatia usafi na hifadhi ya shule wakati wote na kila mahali.
7. Kushiriki,kuthamini na kuheshimu kazi zote halali zitakazotolewa na uongozi wa shule.
8. Kuhudhuria shule na vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.

(Mwanafunzi ambaye ataonyesha dalili zozote za utovu wa nidhamu ataondolewa shuleni bila huruma).

Jina la mwanafunzi_____Saini_____
Jina la mzazi au mlezi_____Saini_____
Tarehe _____Namba ya simu_____

KIAMBATANISHO "B"

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING

MEDICAL EXAMINATIONS FORM

Full Name …….

Age……Height (In Cm) ……. Weight……

1. Blood Count (Red and White) …….
2. Stool Examination…….
3. Urine Analysis……...
4. Syphilis and other V.D……..……..
5. T.B and Leprosy Test……..……..
6. Eye Test……..……..
7. Ears Test……..……..
8. Chest Test……..……..
9. Abdominal Test…….
10. Plano Test (Girls)……...…….
11. Spleen……..……

Additional Information E.G Physical Defects of Impairments Infection Chronic or Family Disease (e.g., Sickle Cell) Inability to eat certain foods Etc.

……
……
……
……
……
……
……

I certify that the above-named Student is Fit/Unfit to Pursue Secondary Education as Stated above.

Signature …….
Designation……
Station……
Date…….